# UJUE UGONJWA WA MNYAUKO WA MIKOROSHO



*Kimetayarishwa na:*

Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania
TARI - Naliendele
S. L. P. 509
MTWARA
Email: cdnaliendele@tari.go.tz

2025

# Ugonjwa wa mnyauko wa Mikorosho

## Utangulizi

Ugonjwa huu ulifahamika rasmi kwa mara ya kwanza mwaka 2012 katika Kijiji cha Magawa, Wilaya ya Mkuranga katika Mkoa wa Pwani. Mwaka 2014 ugonjwa ulionekana katika Kata za Nanganga na Nangoo Wilayani Masasi na Mnongodi katika Wilaya ya Mtwara Vijijini. Ilipofika mwaka 2015 Ugonjwa ulionekana kushambulia mikorosho katika Kijiji cha Tandika, Kata ya Dinduma Wilayani Tandahimba. Ugonjwa huu pia umetolewa taarifa kuwa upo katika baadhi ya sehemu za Mkoa wa Ruvuma.

## Chanzo cha Ugonjwa

Taasisi ya Utafiri wa Kilimo Naliendele kwa kushirikiana na Idara ya Molekyuli Bioteknolojia ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wamefanya Utafiti na kugundua kuwa ugonjwa huu unasababishwa na Vimelea aina ya Uyoga vinavyojulikana kama ***Fusarium oxysporum*** vinavyo ishi kwenye udongo.

## Kusambaa kwa Ugonjwa

Vimelea vya ugonjwa huu husambazwa na shughuli zote za shambani ambazo zinahamisha udongo ulioathirika toka sehemu moja na kupeleka sehemu nyingine, kama vile matumizi ya majembe ya mkono au trekta.


## Dalili za Ugonjwa

- Majani katika baadhi ya Matawi hupoteza rangi yake ya kawaida ya kijani na kubadilika kuwa njano na baadae kahawia.

- Mkorosho ulioathirika ukitazamwa toka mbali unaonekana kuwa na mchanganyiko wa majani ya kijani, njano na kahawia.



- Sehemu ya kati ya mizizi ya mikorosho iliyoshambuliwa na Ugonjwa huu huwa na rangi ya kahawia.



- Hatimaye mti wote hupukutisha majani na kukauka.



**Athari inayoletwa na vimelea hivi**

- Vimela huziba mirija inayopitisha maji na virutubisho toka ardhini kwenda katika majani.

- Pia inaziba mirija inayopitisha chakula toka kwenye majani na kusambazwa katika sehemu mbali mbali za mkorosho.

- Hivyo hatimaye hufanya chakula kisitengenezwe na hata kile kidogo kinachotengenezwa kishindwe kusambazwa.

- Matokeo yake mkorosho unakufa.

## Uhusiano na mabadiliko ya hali ya hewa

- Vimelea aina ya fangasi "*Fusarium oxysporum*" vinafahamika kuishi ardhini na kushambulia aina nyingi za mimea.

- Vimelea hivi vina uwezo wa kuishi katika udongo kwa kipindi kirefu sana katika maeneo yanayotumika kwa kilimo pia na yale yasiyotumika.

- Mabadiliko ya hali ya hewa ndio kufanya vimelea hivi kuanza kushambulia mikorosho.

- Joto linapokuwa zaidi ya nyuzi joto 30 Centigrade na unyevu nyevu zaidi ya 70% hufanya vimelea hivi kuzaliana kwa uwingi na kusababisha ugonjwa.

## Njia za kukabiliana na Ugonjwa

- Usitumie mbegu/miche toka kwenye mashamba ambayo yameathirika.

- Vifaa vya shambani kama vile jembe, panga n.k. ni lazima visafishwe au kupitishwa baada ya kutumika ili kuzuia kuhamisha ugonjwa toka sehemu moja hadi nyingine.

- Dumisha usafi kwenye shamba lako

- Mkorosho ulioathirika ukatwe kisha uchomwe moto kama sehemu ya tahadhari.

- Kazi za kuchunguza njia za kupambana na ugonjwa huu zinaendelea ikijumuisha njia mbalimbali kama vile njia za kikemikali (matumizi ya viuatilifu), njia ya asili/sango na kibailojia.

- Toa taarifa mapema pale unapobaini dalili za ugonjwa huu kama vile njano kwenye majani.